# Utendaji katika Vichekesho Vinavyowasilishwa kwa Njia ya Elektroniki: Uchunguzi wa Vichekesho vya *Ze Orijino Komedi*

**Christopher B. Lucas**
**Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Mt. Augustino**

chrislucas04423@live.com

na

**Maulid Seleman**
**JamiiForums**

mawlidsuleyman@gmail.com

**Ikisiri**
Makala hii imelenga kujadili mbinu za kiutendaji katika vichekesho vinavyowasilishwa kielektroniki. Uchunguzi huu ulichochewa na mgongano wa mawazo kuhusu sifa ya utendaji inavyoathiriwa na mabadiliko ya uwasilishaji wa kazi za fasihi, hususani fasihi simulizi. Data za makala hii zilikusanywa kutoka katika vichekesho teule vya *Ze Orijino Komedi* vilivyohifadhiwa katika mtandao wa *YouTube*. Data hizo zilifafanuliwa na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo huku tukiongozwa na Nadharia ya Utendaji iliyoasisiwa na Dan-Ben-Amos (1972). Nadharia hii imetuongoza kubaini mbinu mbalimbali za kiutendaji zilizotumika katika vichekesho teule vya *Ze Orijino Komedi* vilivyo katika mtandao wa *YouTube*. Matokeo yameonesha uwasilishaji wa vichekesho kwa njia ya elektroniki umesababisha fanani na hadhira kutokuonana ana kwa ana. Hata hivyo, utendaji katika kazi hizi umeendelea kuwapo. Matokeo haya yalifikiwa kutokana na kujitokeza kwa vipengele mbalimbali vya kiutendaji kama vile matumizi ya ishara, uigizaji wa sauti na matendo, matumizi ya maleba, matumizi ya muziki, ushiriki wa hadhira na matumizi ya lugha ya kisanaa.

Kutokana na matokeo hayo, imehitimishwa kwamba mabadiliko ya uwasilishaji wa kazi za fasihi, hususani fasihi simulizi, si uasi bali yanadhihirisha uhai wake. Aidha, uhai huo unatokana na uwezo wa fasihi kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia bila kupoteza sifa ya utendaji.

**Dhana za Msingi:** Vichekesho, Utendaji, Tamthilia, Elektroniki na uwasilishaji

## Utangulizi

Vichekesho au futuhi ni utanzu wa tamthilia ambao una historia ndefu tangu enzi za Aristotle (Kavoi, 2019). Sifa kubwa inayopambanua utanzu huu ni utendaji ambao huibua kicheko kwa hadhira (Ponera, 2010). Sifa ya utendaji inatumika kupambanua utanzu huu kwa sababu vichekesho vya awali vilitegemea matendo yaliyotendwa jukwaani mbele ya hadhira. Hata hivyo, kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, vichekesho vilianza kuwasilishwa kwa njia ya maandishi na, baadaye, katika njia mbalimbali za kielektroniki kama vile redio, runinga na vifaa vingine vya kidijitali. Mabadiliko ya uwasilishaji wa tanzu mbalimbali za fasihi, hasa fasihi simulizi yamezua mitazamo miwili inayokinzana. Mtazamo wa kwanza unaona kuwa uwasilishaji wa tanzu za fasihi zilizokuwa zikitendwa mbele ya hadhira, zama hizi za kutumia njia za kisasa huweza kupoteza sifa ya utendaji wa kazi husika (Amuka, 1991; Thomas, 2005; Mrikaria, 2007; Alex, 2011 na Mlaga, 2017). Mtazamo wa pili unaona kuwa uhifadhi wa tanzu hizo katika njia za kisasa hauathiri sifa ya utendaji (Mutembei, 2006, Ganyi, 2013, Turin na Wheeler, 2013; Gugane, 2014; na Isong, 2018). Mkinzano huu wa mawazo ulitusukuma kuchunguza kipengele cha utendaji katika vichekesho vya Kiswahili kwa kuegemea katika vichekesho vya *Ze Orijino Komedi* vinavyowasilishwa katika njia za kielektroniki. Tulilenga kuchunguza mbinu mbalimbali za kiutendaji katika vichekesho hivyo.

Msokile na Mdee (1984) wanaeleza kuwa utendaji katika kazi za sanaa unajumuisha matendo yanayofanyika, aghalabu, mbele ya hadhira wakati wa uwasilishaji wa simulizi au igizo fulani. Naye Okpewho (1992) anaeleza kuwa utendaji katika kazi ya fasihi ni jumla ya matendo yote pamoja na muktadha mzima unaohusika wakati wa utoaji wa kazi za sanaa. Fasili za wataalamu hawa zinaibua hoja kuwa utendaji ni kiungo muhimu katika kazi za kifasihi zinazowakutanisha fanani na hadhira ana kwa ana. Yamkini, hoja hii ndio iliyomfanya Finnegan (2012) kudai kuwa utendaji ni uti wa mgongo wa kazi yoyote ya fasihi simulizi.

Maelezo yaliyotolewa katika sehemu hii yanaonesha dhana ya utendaji ilivyo muhimu kwa kazi zinazowasilishwa kwa kukutanisha fanani na hadhira ana kwa ana. Hata hivyo, kuna baadhi ya kazi za fasihi simulizi ambazo zimepokea mabadiliko ya uwasilishaji kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ambapo fanani na hadhira hawakutani pamoja. Vichekesho ni utanzu mojawapo ambao umepokea mabadiliko hayo. Hivyo, kulikuwa na haja ya kuhakiki vichekesho vinavyowasilishwa kwa njia ya elektroniki ili kubaini ujitokezaji wa utendaji katika vichekesho hivyo.

Kwa upande mwingine, Dover (1968) anaeleza kuwa vichekesho, kama aina ya drama, vilianza katikati ya mwaka 486 KK huko Syracuse katika mji wa Cicily uliopo nchini Uyunani. Sambamba na hilo, Green (1977) anaweka bayana kuwa vichekesho vilitokana na sherehe za matambiko ya kumtukuza mungu wa mvinyo na rutuba aliyeitwa Dionysus kutoka nchini Uyunani. Utoaji wa vichekesho hivyo uliambatana na matendo mbalimbali yaliyokuwa yakilenga kumtukuza mungu huyo wa mvinyo. Maelezo haya yanaweka msisitizo katika utendaji kama kitu cha msingi katika utanzu wa

vichekesho tangu awali, swala ambalo linaibuka hata katika vichekesho vya Kiswahili.

Mlama (2003) anaeleza kuwa vichekesho vya Kiswahili viliibuka wakati wa ukoloni wa Waingereza na vilikuwa vikitungwa na kuwasilishwa papo kwa papo. Lihamba (1985), akifafanua zaidi kuhusu vichekesho vya kidrama, anaeleza kuwa wakati wa ukoloni wa Waingereza, ulianzishwa uigizaji wa majukwaani, ambapo vichekesho hivyo vilifanywa shuleni na vingine vilifanywa na vikundi vya mtaani katika shughuli mbalimbali. Kimsingi, uwasilishaji wa vichekesho mbele ya hadhira au wa jukwaani unaofafanuliwa na Mlama na Lihamba, uliambatana na matendo mbalimbali ambayo ni sehemu muhimu ya ukamilifu wa utanzu wa vichekesho kifani na kimaudhui. Akifafanua zaidi kuhusu sifa hiyo ya utendaji katika vichekesho, Ponera (2014) anaeleza kuwa miongoni mwa sifa na vijenzi muhimu vya vichekesho ni kuwapo kwa utendaji ambao hufanyika jukwaani au mbele ya hadhira. Mawazo ya Ponera yanadokeza kimajumui namna utendaji ulivyo kiambajengo muhimu katika uwasilishaji wa vichekesho.

Fauka ya hayo, wakati wa Azimio la Arusha, njia za uwasilishaji wa vichekesho ziliongezeka. Mulokozi (1996) anafafanua kuwa, katika zama hizi, vichekesho vilianza kutendwa kupitia vipindi mbalimbali vya redioni. Aidha, Mulokozi anaweka bayana kuwa kulikuwa na vichekesho maarufu vilivyofanyika katika Redio Tanzania kama vile *Mahoka* kilichoanza mwaka 1974, na *Pwagu na Pwaguzi* kilichoanza mwaka 1978. Mawazo ya mtaalamu huyu yanadokeza kuwa, wakati wa Azimio la Arusha, uwasilishaji wa vichekesho ulibadilika na kuanza kuwasilishwa kwa njia ya redio. Samwel (2013) na Mulokozi (2017) wanaeleza kuwa, kutokana na

maendeleo ya teknolojia katika jamii, umeibuka mkondo mpya wa uwasilishaji wa vichekesho unaofanywa na baadhi ya vikundi kama *Vioja Mahakamani* na *Ze Komedi* kupitia televisheni. Mabadiliko ya uwasilishaji wa vichekesho vya Kiswahili kama kazi nyingine za kifasihi yanazua mitazamo miwili inayokinzana. Mtazamo wa kwanza ni ule unaoungwa mkono na Amuka (1991), Thomas (2005), Mrikaria (2007), Alex (2011) na Mlaga (2017) ambao wanaona kuwa uwasilishaji wa kazi za fasihi kwa kutumia vifaa vya kielektroniki umesababisha kazi hizo kukosa ladha yake halisi, hivyo, kupoteza sifa muhimu ya utendaji. Mtazamo wa pili unaungwa mkono na Mutembei (2006), Ganyi (2013), Turin na Wheeler (2013), Gugane (2014) na Isong (2018) ambao wanaeleza kuwa kazi za fasihi zinazowasilishwa kwa kutumia vifaa vya kielektroniki hazijapoteza sifa ya utendaji kwa sababu vifaa hivi vinawezesha matendo yanayofanyika wakati wa utoaji wa tanzu. Kusigana kwa mawazo kuhusu mabadiliko ya uwasilishaji wa vichekesho kunatupa shauku ya kuchunguza mbinu za kiutendaji katika vichekesho vinavyowasilishwa kwa njia ya televisheni, hasa vichekesho vya *Ze Orijinal Komedi* ili kubaini mbinu mbalimbali za utendaji.

*Ze Orijino Komedi* ni kikundi cha uchekeshaji. Kilianza kurusha vichekesho vyake kwa njia ya televisheni kupitia *East Africa Televisioni* (EATV) baadaye Shirika la Utangazaji la Tanzania (TBC1) na sasa katika *DSTV*. Kikundi cha *Ze Orijino Komedi* kinasambaza vichekesho vyake kupitia mtandao wa *YouTube*. Kikundi cha *Ze Orijino Komedi* kinaundwa na waigizaji sita ambao ni Lucas Mhuvile (Joti), Mujuni Sylivester (Mpoki), Emanuel Mgaya (Masanja Mkandamizaji), Emanuel Mwakilasa (Wakuvwanga), Joseph Shamba (Vengu) na Alex Chalamila (Macregan).

Hivyo, katika makala hii tulifanya uchunguzi wa mbinu za kiutendaji zinazotumiwa na kikundi hiki.

**Nadharia ya Utafiti**

Hii ni nadharia inayoshughulika na uwasilishaji wa kazi za fasihi simulizi kwa kuzingatia muktadha unaohusisha ushiriki wa fanani na hadhira (Mulokozi, 2002). Nadharia hii iliasisiwa na Dan-Ben-Amos (1972) na kuendelezwa na Bauman (1975). Aidha, Nadharia ya Utendaji ilichota mawazo kutoka katika taaluma mbalimbali kama vile Anthropolojia, Isimu, na Fasihi. Akifafanua zaidi kuhusu nadharia hii, Bauman anaeleza kuwa, katika kutumia Nadharia ya Utendaji, wahakiki wa kazi za sanaa wanapaswa kuzama katika matini zaidi ya moja ya fasihi ili kubaini utendaji unaoenda sambamba na matini husika. Nadharia ya Utendaji iliungwa mkono na wataalamu mbalimbali, akiwamo Schechner (2013).

Bauman (1975) anataja mihimili minne ya Nadharia ya Utendaji. Mihimili hiyo ni matumizi ya lugha ya kipekee*,* fomyula simulizi, matumizi ya lugha ya picha za kisanaa, na mbinu rasmi za kiutendaji. Katika kutumia nadharia hii, makala hii imechunguza vichekesho vya *Ze Orijino Komedi* kwa kuzingatia msingi wa mbinu rasmi za kiutendaji kama ulivyobainishwa na Bauman *(khj)*. Msingi huu unafafanuliwa vyema na Okpewho (1992) kwa kueleza kuwa utendaji katika kazi za kifasihi simulizi hauishii katika matumizi ya maneno pekee, bali huweza kujitokeza kupitia viziada lugha. Okpewho *(khj)* anafafanua kuwa viziada lugha huhusisha mambo mbalimbali yanayofanywa na viungo vya mwili kama vile matumizi ya ishara, sauti, muziki, uchezaji, na uigizaji. Hivyo, msingi huu utatuongoza kumulika mbinu mbalimbali za kiutendaji katika vichekesho teule.

## Methodolojia

Makala hii imetumia data za maktabani, ambapo vichekesho vya *Ze Orijino Komedi* vilivyohifadhiwa katika mtandao wa *YouTube* vimechunguzwa. Aidha, usampulishaji lengwa ulitusaidia kupata vichekesho kumi ambavyo tumevitumia katika makala hii ambavyo ni "Ndoa Ndoano1", "Mjumbe wa Mtaa vs Mhamiaji", "Mama Ima aita Tax Kijijini", "Timbwili Timbwili la Asha Ngedere", "Orijino Komedi na Amefulia", "Mchanganuo wa Rambirambi", "OK Kukopi na Kupest", "Mpoki na Karina", "Orijino Komedi walivyoingia kwenye Harusi ya Masanja", na "Pritenda". Data katika vichekesho hivyo zilikusanywa kwa njia ya utazamaji wa vichekesho na upitiaji nyaraka. Data hizo zilichanganuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli.

## Matokeo ya Utafiti

Matokeo yanaonesha kuwa kuna mbinu kuu nne za kiutendaji katika vichekesho teule vya *Ze Orijino Komedi.* Kwa kuongozwa na msingi wa mbinu rasmi za kiutendaji katika Nadharia ya Kiutendaji, makala hii imebaini kuwapo kwa matumizi ya mbinu ya uigizaji, mbinu ya uimbaji wa nyimbo, na uchezaji wa muziki, matumizi ya ishara, na mbinu ya ushirikishwaji wa hadhira.

## Mbinu ya uigizaji

Uigizaji ni mbinu maridhawa ya kuwasilisha kazi mbalimbali za kifasihi. Mbinu hii hutumika katika uwasilishaji wa tanzu mbalimbali za fasihi simulizi pale fanani wanapoiga tabia na matendo ya watu au viumbe wengine waliopo katika jamii. Akifafanua zaidi hoja hii, Wamitila (2010) anasema kuwa mbinu ya uigizaji humwongoza msanii au mtendaji kuwasilisha, kutenda matendo mbalimbali, au kumithilisha tabia za watu mbalimbali waliopo katika jamii. Utafiti huu umebaini kuwa mbinu ya

uigizaji katika vichekesho vya *Ze Orijino Komedi* imejitokeza kupitia uigaji wa sauti na matendo pamoja na matumizi ya matendo unyume.

***Mbinu ya uigaji wa sauti na matendo***

Kupitia makala hii, tumebaini kuwa, wakati wa uwasilishaji wa kazi za kifasihi, wasanii (fanani) huigiza sauti na matendo ya watu mbalimbali kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa hadhira waliyoikusudia. Abrams (1999), akifafanua hoja ya makala hii, anaeleza kuwa, wakati wa utoaji wa kazi ya kisanaa, watendaji huiga tabia au mienendo ya watu na viumbe waliopo katika jamii ili kusisitiza kile walichokikusudia kukielezea kuhusu watu hao. Katika vichekesho teule vya *Ze Orijino Komedi*, mbinu ya uigaji sauti na matendo imejitokeza katika kichekesho cha "Mpoki na Karina" pamoja na kichekesho cha "Pritenda" kama ifuatavyo:

Katika kichekesho cha "Mpoki na Karina", tunaoneshwa msanii Mpoki akiigiza sauti na matendo ya hayati John Komba[1]. Katika uigaji huu, Mpoki anaigiza namna ya uongeaji na uchekaji wa hayati John Komba ili kuleta kufanana na kiongozi huyo. Vilevile, katika uigaji huu, tunaoneshwa mhusika Mpoki akitumia mavazi na mapambo maalumu ili kupata baadhi ya sifa za mwonekano aliokusudiwa. Kutokana na hali hiyo, makala hii inabainisha kuwa mbinu ya uigaji wa sauti na matendo iliyotumika katika kichekesho hiki imelenga kuvuta umakini wa hadhira. Mbinu hii imeiwezesha hadhira kuelewa mhusika anayekusudiwa kuelezewa ili

[1] Komba alikuwa msanii wa nyimbo mbalimbali za kisiasa zilizowahi kuvuma nchini Tanzania kama vile wimbo uitwao "kama sio juhudi zako Nyerere", na wimbo wa CCM uitwao "CCM Mbele kwa Mbele". Pia msanii huyu alikuwa mbunge wa Mbinga Magharibi kuanzia mwaka 2010 mpaka mwaka 2015. Mbunge huyu alifariki mwaka 2015 akiwa bado na cheo cha Ubunge wa Mbinga Magharibi.

kuweka msisitizo wa jambo lililokusudiwa kuwasilishwa kuhusu mhusika anayerejelewa.

Kadhalika, katika kichekesho cha "Pritenda" mbinu ya uigaji wa sauti na matendo imetumiwa na mhusika Masanja Mkandamizaji. Katika kichekesho hiki, Masanja anaoneshwa akiiga sauti na namna ya uongeaji wa hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Vilevile, Masanja anatumia vifaa kama fimbo pamoja na kupaka rangi nyeupe kwenye nywele ili kupata sifa na mwonekano halisi wa Mwalimu Nyerere. Hivyo, katika makala hii, tunaona kuwa uigaji wa sauti na matendo uliofanyika katika kichekesho cha "Pritenda" umelenga zaidi kumuenzi Mwalimu Nyerere kwa kusisitiza masuala mbalimbali aliyokuwa akiyapa kipaumbele enzi za uhai wake. Zaidi ya hayo, tunaona kuwa uigaji wa sauti na matendo umetumika kama kionjo cha kisanaa kilicholenga kuvuta umakini pamoja na kuifurahisha hadhira inayotazama kichekesho hiki. Kwa msingi huo, inaonesha kuwa wachekeshaji huiga sauti na matendo ya watu mbalimbali ili kuvuta umakini wa hadhira pamoja na kuenzi au kukataza tabia fulani zinazofanywa na wahusika hao wanaoigwa.

***Mbinu ya matendo unyume***

Matendo unyume ni mbinu ya kiutendaji ambayo inatumika wakati wa uwasilishaji wa vichekesho, ambapo wahusika hutenda matendo ambayo yapo kinyume na mwonekano au mavazi waliyotumia mbele ya hadhira. Beez (2004) anaeleza kuwa, wakati wa utendaji wa kazi ya kifasihi, kuna mambo mbalimbali ambayo huweza kutokea na kuiacha hadhira katika mshangao. Beez *(khj)* anaongeza kuwa, katika jambo hili, fanani huweza kutenda jambo ambalo lipo kinyume na uhalisia wake. Katika utafiti huu, tumebaini kuwa, katika uwasilishaji wa vichekesho, fanani hufanya mambo

yaliyo kinyume na uhalisia wa mwonekano wake pamoja na mavazi aliyotumia mbele ya hadhira. Hivyo, matendo ya aina hii yanayofanyika katika vichekesho katika utafiti huu yamerejelewa kama matendo unyume. Tukiongozwa na Nadharia ya Utendaji, kupitia msingi wa viziada lugha, utafiti wetu ulibaini kuwa mbinu ya matendo unyume katika vichekesho teule vya *Ze Orijino Komedi* imejitokeza katika kichekesho cha "Orijino Komedi katika Harusi ya Masanja". Katika kichekesho hiki, tunaoneshwa Joti, Wakuvwanga na Macregan wakiingia ukumbini kwa mwendo wa gwaride huku wakiwa kwenye mavazi ya kiaskari. Wakiwa katika mwonekano wa askari, wahusika hawa wanatenda matendo yaliyo kinyume na mavazi ya kiaskari kwa kucheza muziki kwa mtindo wa kukata viuno mbele ya hadhira.



**Kielelezo Na. 1: Wasanii wa *Ze Orijino Komedi* wakicheza muziki huku wamevaa nguo kama askari (Chanzo: *YouTube*)**

Katika kielelezo hiki, tunaoneshwa wahusika wakicheza muziki huku wakiwa wamevaa mavazi kama ya kiaskari. Kimsingi, katika utafiti huu, tumeona kuwa kichekesho cha "Orijino Komedi Wakiingia kwenye Harusi ya Masanja" kimetumia mbinu ya matendo unyume kutokana na kanuni na mamlaka ambayo askari wamejijengea katika jamii yetu. Ni vigumu kuwakuta wakiwa wanacheza kwa mitindo hiyo mbele ya hadhira. Sambamba na hilo, kumekuwa na adhabu mbalimbali ambazo zimekuwa

zikitolewa kwa askari ambao wanafanya vitendo ambavyo ni kinyume na kanuni za kazi zao wakiwa katika sare za kazi. Hivyo, katika utafiti huu, tunaona kwamba mbinu ya matendo unyume imetumiwa kwa makusudi na wasanii hawa kwa lengo la kuibua taharuki na kufurahisha hadhira iliyohudhuria harusi ya msanii mwenzao.

**Mbinu ya uimbaji wa nyimbo na uchezaji wa muziki**

Mbinu ya utendaji ya matumizi ya muziki ni miongoni mwa vipengele vya kiutendaji vinavyotokana na msingi wa viziada lugha. Katika makala hii, msingi wa viziada lugha umetuongoza kuchunguza namna matumizi ya muziki yanavyojitokeza katika uwasilishaji wa vichekesho. Makala hii inabainisha kuwa mbinu ya matumizi ya muziki katika vichekesho teule vya *Ze Orijino Komedi* imejitokeza kupitia uimbaji wa nyimbo unaoenda pamwe na uchezaji wa muziki. Baadhi ya wataalamu wanaeleza kuwa, wakati wa utendaji wa kazi ya kisanaa, wasanii huweza kuimba na kucheza kwa vionjo mbalimbali kwa lengo la kuchangamsha hadhira au kufikisha ujumbe fulani (Mlama na Balisidya, 1976 na Rashid, 2016). Utafiti wetu ulibaini kuwa, katika vichekesho teule vya *Ze Orijino Komedi,* mbinu ya uimbaji na uchezaji wa muziki imejitokeza katika kichekesho kinachoitwa "Kukopi na Kupesti" na "Mama Ima Aita Tax Kijijini."

Katika kichekesho cha "Kukopi na Kupesti", uimbaji wa wimbo umefanywa na mhusika Joti na Macregani. Wahusika hao wanaoneshwa wakiimba sehemu ndogo ya wimbo unaoitwa "Mapenzi Kitu Gani" ulioimbwa na kikundi kinachoitwa *FM Academia.* Mhusika Joti anaanza kwa kumsifia Macregani kwa utunzi bora wa wimbo bila kutaja jina la msanii aliyekusudiwa kuongelewa. Katika maongezi haya, mhusika Joti anaanza kuimba sehemu ndogo ya wimbo unaoitwa "Mapenzi Kitu Gani"

huku akicheza kwa mtindo wa kukata kiuno na kupiga makofi huku Macregan akimuunga mkono. Maoni yetu ni kwamba mbinu ya uimbaji na uchezaji wa muziki iliyotumika katika kichekesho hiki imekusudia kuburudisha pamoja na kuondoa sintofahamu kwa hadhira juu ya msanii anayeongelewa. Hivyo, matumizi ya muziki katika kichekesho hiki yametumika kama kiungo muhimu baina ya fanani na hadhira ili kulielewa jambo linalozungumziwa.

Kadhalika, katika kichekesho cha "Mama Ima Aita Tax Kijijini," uimbaji wa wimbo umefanywa na mhusika Masanja Mkandamizaji na Wakuvwanga. Katika kichekesho hiki, Masanja Mkandamizaji anaoneshwa akiwa amefurahi kupata taarifa ya kwenda mjini kwa taksi, ambapo furaha hiyo inasababisha aimbe na kucheza wimbo uitwao "Amekong'otwa". Kutokana na Masanja kuimba wimbo huo, Wakuvwanga anavutiwa na kuamua kuungana naye katika kuimba pamoja na kucheza wimbo huo. Matumizi ya mbinu ya uchezaji na uimbaji wa wimbo katika kichekesho hiki yamekusudia kuchangamsha na kuvuta umakini kwa hadhira kuendelea kufuatilia kichekesho hiki. Wakifafanua zaidi hoja hii, Okpewho (1992), Askew (2002) Omari (2009) na Brunott (2013) wanaeleza kuwa, katika utendaji, matumizi ya nyimbo husaidia kuleta uhai na kuchangamsha hadhira kutokana na kusheheni vionjo mbalimbali vinavyowaburudisha. Hivyo, utafiti wetu umebaini kuwa nyimbo nyingi zinazoimbwa au kutumika katika vichekesho ni zile zinazojulikana na kupendwa sana na hadhira ikiwa kama sehemu mojawapo ya kuishirikisha hadhira kwa kuimba au kucheza wimbo husika. Kwa msingi huo, endapo wasanii wangekuwa wanaimba nyimbo ambazo hazifahamiki kwa hadhira zao

ingeiwia vigumu hadhira kushiriki katika uimbaji na kuelewa kile kilichokusudiwa na watendaji.

**Mbinu ya matumizi ya ishara**

Abrams (1999) anaeleza kuwa ishara ni lugha zinazoendana na vidokezo mbalimbali vya matumizi ya viungo vya mwili kama mikono, uso, na kichwa. Katika msingi wa viziada lugha, matumizi ya ishara ni miongoni mwa vipengele vinavyojenga utendaji katika kazi za fasihi kupitia ishara za uso, miondoko ya mwili na mavazi. Katika makala hii, tumebaini kuwa matumizi ya ishara katika vichekesho vya *Ze Origino Komedi* yamejitokeza kupitia matumizi ya maleba (mavazi) pamoja na mbinu ya ububu.

***Mbinu ya matumizi ya maleba***

Musgrove (2003) anaeleza kuwa maleba ni jumla ya mavazi na mapambo mbalimbali yanayotumika wakati wa uwasilishaji wa kazi ya kisanaa. Utafiti huu umebaini kuwa maleba ni miongoni mwa vipengele muhimu wakati wa utendaji wa vichekesho. Vichekesho vya "Ndoa Ndoano1", "Mama Ima Aita Tax Kijijini", "Timbwili Timbwili la Asha Ngedere" na "Mpoki na Karina" vimeweza kuonesha mbinu hii inavyojitokeza.

Katika kichekesho cha "Ndoa Ndoano1", "Mama Ima Aita Tax Kijijini", na "Timbwili Timbwili la Asha Ngedere" wahusika Wakuvwanga, Macregan na Joti wametumia maleba, yaani mavazi ya kike kama vile gauni, sidiria, wigi pamoja na kutumia mapambo ya wanawake kama vile wanja na lipstiki ili kuvaa na kupata mwonekano wa mwanamke. Matumizi ya maleba ya kike katika vichekesho hivi yamelenga kuwawezesha wasanii wa kikundi hiki kuendana na muktadha uliokusudiwa kuwasilishwa. Zaidi ya hayo, utafiti huu unaona kuwa maleba yaliyotumika katika vichekesho hivi yamelenga kuburudisha na kuchekesha hadhira kutokana na mavazi ya kike

kuvaliwa na wahusika wa kiume. Katika kuthibitisha hoja hii, Wamitila (2002) anafafanua kuwa, katika vichekesho, wasanii huwaburudisha hadhira na kuwaletea kicheko kutokana na wahusika wa kiume kuvaa mavazi ya kike. Hivyo, matumizi ya maleba ya kike katika vichekesho hivi yametumiwa na wahusika ili kubeba uhalisia wa muktadha wa jambo wanaloliwasilisha pamoja na kuburudisha hadhira inayowatazama.

***Mbinu ya matumizi ya ububu (igizo-bubu)***

Ububu ni matumizi ya mbinu ya kiutendaji ambayo inahusisha matumizi ya matendo peke yake bila kutumia maneno. Katika kufafanua zaidi hoja hii, Abrams (1999) anaeleza kuwa, katika uwasilishaji wa kazi ya kifasihi, fanani huweza kutenda matendo mbalimbali pasipo kutumia maneno, lakini matendo hayo yakaleta maana kwa hadhira yake. Katika vichekesho teule vya *Ze Orijino Komedi,* mbinu ya maimu imetumika katika kichekesho kinachoitwa “Ndoa Ndoano1”.

Katika kichekesho cha “Ndoa Ndoana1”, mbinu ya ububu imetumiwa na mhusika Wakuvwanga na Macregani. Katika kichekesho hiki, tunaoneshwa matendo mbalimbali yanafanywa na Macregani na Wakuvwaga pasipo kuzungumza neno lolote mwanzo hadi mwisho wa kichekesho. Mathalani, kichekesho kinaanza Macregani akifua nguo zake akiwa nje ya nyumba, kisha anaoneshwa Wakuvwanga akitoka ndani akiwa ameshika nguo chafu mkononi na kuzirushia kwa Macregani bila kuzungumza chochote. Naye, Macregani anazichukua nguo hizo na kuzirusha pembeni kwa hasira bila kuzungumza chochote. Pamoja na kuwa kichekesho hiki hakijatumia maneno yoyote, katika utafiti huu, tunaona kwamba mbinu ya kimya iliyotumika katika kichekesho hiki inaashiria kutokuwapo kwa maelewano baina ya wenza [mke na mume] kutokana na matendo hayo wanayofanyiana.

Hivyo, kutokana na matumizi ya mbinu hii, utafiti wetu umebaini kuwa si lazima vichekesho vijengwe kupitia maneno au majibizano ya wahusika. Wakati mwingine, vichekesho huweza kujengwa kupitia matendo peke yake bila kutumia maneno. Akifafanua zaidi kuhusu hoja hii, Mutembei (2012) anaeleza kuwa mbinu ya ukimya inajitokeza pale ambapo msanii anatumia matendo peke yake bila kutumia sauti, lakini matendo hayo huwa na athari na maana fulani kwa watazamaji au wasikilizaji wa kazi ya kisanaa. Mutembei *(khj)* anaongeza kuwa matumizi ya mbinu ya kimya husaidia katika kuifikirisha hadhira juu ya tukio linalotendwa na wasanii husika.

**Mbinu ya ushiriki wa hadhira**

Msingi wa viziada lugha unasisitiza hadhira kushiriki katika kazi ya sanaa kwa kuongozwa na matendo mbalimbali yanayofanywa na fanani. Hadhira huweza kushiriki kwa kuonesha hisia za furaha au huzuni, kujibu maswali, kuitikia wimbo na kutoa maoni kulingana na tukio linalowasilishwa na fanani. Katika uwasilishaji wa vichekesho, ushiriki wa fanani unajidhihirisha zaidi katika vichekesho vinavyowasilishwa papo kwa papo au jukwaani. Akifafanua zaidi hoja hii, Bakary (2016) anaeleza kuwa, katika vichekesho vya jukwaani, hadhira hushiriki kwa kucheka, kupiga makofi na kutenda matendo mbalimbali kulingana na matendo yanayofanyika jukwaani. Hata hivyo, kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, imekuwa si lazima ushiriki wa hadhira katika kazi ya sanaa uhusishe kukutana ana kwa ana kati yake na fanani. Akifafanua zaidi hoja hii, Mutembei (2006) anaeleza kuwa maendeleo ya sayansi na teknolojia yameondoa ulazima wa fanani na hadhira kukutana wakati wa uwasilishaji wa kazi ya sanaa. Katika utafiti huu, tumebaini kuwa, ijapokuwa fanani na hadhira hawawi pamoja wakati wa uwasilishaji wa vichekesho vilivyopo

katika mtandao wa *YouTube*, ushiriki wa hadhira katika vichekesho hivyo unaendelea kwa namna zifuatazo:

Kwanza, hadhira hushiriki kwa kuonesha ishara ya kupenda au kutopenda jambo lililowasilishwa na fanani. Uwasilishaji wa vichekesho katika mtandao wa *YouTube* unawawezesha hadhira kushiriki katika kazi hiyo kwa kuonesha hisia zao kama wamefurahishwa au kuchukizwa na namna kazi husika ilivyowasilishwa na fanani. Katika kufanikisha jambo hilo, mtandao wa *YouTube* una vitufe viwili maalumu ambavyo huipa hadhira nafasi ya kuchagua kubonyeza kimojawapo kuonesha hisia zao juu ya jambo linalotendwa na fanani. Katika vichekesho teule vya *Ze Orijino Komedi* vilivyopo katika mtandao wa *YouTube*, hadhira imeshiriki kwa kuonesha hisia zao kwa kubonyeza vitufe vinavyoendana na hisia zao kuhusu kichekesho kinachowasilishwa. Mathalani, katika kichekesho cha "Mjumbe wa Mtaa vs Mhamiaji" hadhira imeshiriki kwa kubonyeza vitufe vilivyoendana na hisia zake kuhusu kichekesho hicho. Jambo hili linajidhihirisha katika kielelezo Na. 2 kifuatacho:




**Kielelezo Na. 2: Alama ya Ushiriki wa Hadhira (Chanzo: *YouTube*)**

Kielelezo hiki kinaonesha namna hadhira ilivyoshiriki kwa kuonesha hisia zake katika kupenda au kutopenda kile kilichowasilishwa. Kisanduku kinaonesha kuwa watu elfu mbili mia moja walipendezwa na kichekesho hicho wakati duara linaonesha watu mia tatu hawakupendezwa na kichekesho husika. Hivyo, mrejesho wa watu waliopenda na wasiopenda humpa fanani nafasi ya kujitathmini na kujua namna ambavyo hadhira imepokea kazi yake.

Pili, hadhira hushiriki kwa kuandika maoni yake kuhusu jambo lililowasilishwa. Mtandao wa *YouTube* unaipa hadhira fursa ya kushiriki katika kazi ya sanaa kupitia kutoa maoni mbalimbali juu ya kazi iliyofanywa na fanani. Katika kuwezesha jambo hilo, mtandao wa *YouTube* una kisanduku maalumu cha kutolea maoni ambacho kinairuhusu hadhira kuandika maoni yake juu ya jambo lililowasilishwa. Sambamba na hilo, katika mtandao wa *YouTube*, fanani huweza kujibu baadhi ya maoni ambayo anaona yanafaa kujibiwa. Katika vichekesho vya *Ze Orijino Komedi,* ushiriki wa hadhira kupitia utoaji wa maoni umejitokeza katika vichekesho vyote vilivyopo katika mtandao huo. Mathalani, katika kichekesho cha "Pritenda" hadhira imeshiriki kwa kuandika maoni

mbalimbali kuhusu kichekesho hicho. Jambo hili linajidhihirisha katika kielelezo kifuatacho:




**Kielelezo Na. 3: Baadhi ya Maoni Yaliyotolewa na Hadhira katika Kichekesho cha Pritenda (Chanzo: *YouTube*)**

Kielelezo hicho kinaonesha baadhi ya maoni yaliyotolewa na hadhira katika kichekesho kinachoitwa "Pritenda". Japo fanani na hadhira hawawi pamoja wakati wa uwasilishaji wa vichekesho hivyo, lakini hadhira hupata nafasi ya kutoa maoni kuhusu jambo lililowasilishwa na fanani. Hivyo, kupitia maoni hayo, fanani anaweza kuelewa hisia za hadhira juu ya kile alichokiwasilisha. Mathalani, endapo maoni mengi yaliyotolewa na hadhira yatakuwa chanya, itampa nguvu fanani kuendelea kutumia mbinu hiyo kuwasilisha. Kwa upande mwingine, endapo maoni yakiwa hasi itamchochea fanani kubadilisha namna ya uwasilishaji wake katika kazi zinazofuata. Ganyi (2013) anaeleza kuwa uwasilishaji wa kazi za sanaa kwa kutumia vifaa vya kielektroniki unaruhusu ushiriki wa hadhira kupitia utoaji maoni yake kuhusu kazi inayowasilishwa.

Kwa ujumla, kutokana na mbinu za kiutendaji zilizobainishwa na makala hii, tunaunga mkono mawazo ya wataalamu wanaoamini kuwa kuhifadhi na kuwasilisha kazi za fasihi kielektroniki hakupotezi mbinu za kiutendaji katika kazi husika. Makala hii inaona kuwa utendaji unaojitokeza kielektroniki una sifa zote za msingi zinazobainishwa na Nadharia ya Utendaji.

**Hitimisho**

Katika makala hii, tunaona kuwa japo fanani na hadhira hawakutani moja kwa moja wakati wa uwasilishaji wa kazi za kisanaa, hususani kazi zinazowasilishwa kwa kutumia vifaa vya kielektroniki, bado ushiriki wa hadhira unaendelea kuwapo kama ilivyofafanuliwa katika makala hii. Aidha, changamoto kubwa ya ushiriki huu ni kwamba hadhira haihusiki moja kwa moja katika muda ule ambao kazi inawasilishwa. Hata hivyo, hadhira ya mtandao wa *YouTube* huweza kutoa mchango na kuathiri kazi zinazofuata za hadhira kutokana na maoni na hisia zilizooneshwa na hadhira yake. Makala hii inatoa wito kwa watafiti au waandishi wengine kuziangaza mbinu za kiutendaji zinazoitumika kwenye kazi nyingine za kifasihi zinazohifadhiwa katika njia ya kielektroniki ili kubaini mbinu nyingine zaidi ambazo hazikubainika katika vichekesho vilivyoteuliwa.

**Marejeleo**


Abdulla, L.M. (2006). Athari za Itikadi zatika Nyimbo za Harusi za Kizanzibar, (Tasinifu ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Abrams, M.H. (1999). *A Glossary of Literary Terms,* 7th Edition. USA: Earl McPeek.

Alex, G. (2011). *Technology, Literature and Cuture*. Cambridge: Polity Press.

Askew, J. (2002). Perfoming the National Through Swahili Music and Cultural Politics in Tanzania. London: Heinemann.

Dover, K.J. (1968). *Greek Comedy*. Oxford: University of California Press.

Finnegan, R. (2012). *Oral Literature in Africa*. Oxford: The Clarendon Press.

Ganyi, F.M. (2013). The Impact of Technological Development on the Contextual Imperative of Perfomance in the Delivary of Folkrole. *Journal of Humanities and Social Science, Toleo la 11,* 1 - 8.

Gugane, B.R. (2014). *Impact of Technology Advancement on Literature*. Rambhoomi. New Man Publication.

Green, E.J. (1977). *Menander to Marivaux: The History of the Comic Structure*. Alberta: The University of Alberta Press.

Isang, A. (2018). The Influence of New Media Technologies on African Literature, (Unpublished PhD Thesis), The University of De Monfort.

Kabeja, F.M. (2012). Dhima za Ufutuhi katika Riwaya za Shaaban Robert, (Tasinifu ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Lihamba, A (1985). Politics and Theatre in Tanzania after the Arusha Declaratin: 1967 - 1984, (Unpublished PhD Thesis), The University of Leeds.

Lord, A. (1960). *The Singer of Tales.* Cambridge: Havard University Press.

Metthew, B and Ross, R (2010). *Research Methods Practle Guid for Social Science*. London: Pearson.

Mhando, P. & Balisidya, N. (1976). Fasihi na Sanaa za Maonyesho. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mlaga, W. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi, Karne ya 21*. Heko Publihser Ltd.

Mlama, P.O. (2003). Tamthiliya katika Mazingira ya Tanzania. Katika *Makala za Semina za Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III:* 206 - 212.

Mrikaria, E.S. (2007). Fasihi Simulizi na Teknolojia Mpya. Katika *Swahili Forum (14),* kur. 197-206.

Msokile, M. (1992*). Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: DUP.

Muhando, P. Na Balisidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*. Dar es Salaam: TPH.

Muiruri, P.K. (2006). *Maandalizi Muft ya K.C.S.E Fasihi Simulizi, Maswali na Majibu.* Kenya: Palco Enterprises Ltd.

Mulokozi, M. (2002). *The African Epic Controversy: Historicaal, Philosophical and Aesthetic Perspectives on Poetry and Perfomance*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Mulokozi, M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. kazi za Fasihi vyuoni na vyuo Dar es Salaam: KAUTTU.

Musgrove, J. (2003). Makeup, Hair and Customes for Film and Television. Canada: Focal Press.

Mutembei, A.K. (2006). Nadharia ya Fasihi Simulizi na Maendeleo katika Sayansi na Teknolojia. *Mulika.* 27, 1-17

Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature.* Backgrounds, Character, and Continuity. Indiana University Press: USA.

Omari, S. (2009). Hip Hop Music as Popular Oral Poetry, (Unpublished PhD Thesis), The University of Dar es Salaam.

Ponera, A.S. (2010) Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert: Maana yake, Sababu za kutumiwa na Athari zake kwa Wasomaji, (Tasinifu ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu Dodoma.

Ponera, A.S. (2014). Kutoka Futuhi Hadi Ufutuhi: Chimbuko, Maendeleo na Nadharia zake. *Mulika*.33, 1 - 20.

Ross, A. (1998). *The Language of Humor*. New York: Routiledge.

Rashid, H.S. (2016). Kuchunguza Dhima za Nyimbo za Ngoma ya Kibati Mkoa wa Kusini Pemba, (Tasinifu ya Uzamili, haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Samwel, M. (2013). *Tamthiliya ya Kiswahili: Kutoka Miviga ya Kidini hadi Filamu*. Dar es Salaam: Meveli.

Thomas, R (2005). Literature and the Written Word: Lost in Transcription. In *Specia Editors Column* kur 1-6 imesomwa mtandaoni tarehe 13/ 03/ 2019 https://academia.edu>special-editors-column.

Turin, M. and Wheeler, C. (2013). Oral Literature in Digital Age: Archiving Orality and Connecting with Community. Cambridge: Open Book Publisher.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Mombasa: Kenya Litho Ltd.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Kiswahili: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.

Wamitila, K.W. (2004). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi* Focus Publication ltd: Nairobi.

Wamitila, K.W. (2010). *Kanzi za Fasihi: Misingi na Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Ltd.

Westmore, M. (1973). *The Art of Theotrical Makeup for Stage and Screen*. Austria: McGraw-Hill Book Company.